

# *Ukweli Hauna Kutu* Pambazuko

Toleo Namba 011

Jumatatu Septemba 19-25, 2022

**'Wakubwa' wasiongeze mateso barabarani Uk. 2**



**Wamjaribu  
Rais Mwinyi  
Uk. 12**

**Watanzania  
tumuombee  
Lowassa**

**Eacop yajali viwango, EU 'wachemka' Uk. 16**

**JISAJILI HAPA: Andika neno HABARI na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure**

### Wasiungeze mateso barabarani

**T**AARIFA kwamba misafara ya viongozi wakuu wa serikali kusimamisha shughuli za uzalishaji mali katika maeneo wanakopita na ama kulala, siyo ngeni na kamwe siyo uongo.

Watanzania wamekuwa mashuhuda wazuri wa kadhia hii ya kusimamishwa kwa saa kadhaa barabarani – baada ya njia kufungwa, wakisubiri mkubwa mmoja apite. Zipo taarifa pia kwamba wapo wanaozuiwa kuendelea na shughuli zao kwa kuwa anakolala mkubwa ni jirani na shughuli zao, hivyo hulazimishwa kufunga ili mkubwa apumzike kwa usalama.

Pamoja na kwamba hatuna lolote kubwa kwa viongozi wa juu; rais, makamu wake, waziri mkuu na Rais wa Zanzibar, wanapokwenda kwenye shughuli na kulazimisha wanausalama kufunga barabara ama kuzuia magari kusogea, lakini tunabeba kilio cha wananchi wengi wanapooona viongozi wengine wakilazimisha njia kufungwa kwa kuwa na wao wanapita.

Imekuwa ni kawaida, kwa miaka ya hivi karibuni wananchi kusimamishwa kwa muda mrefu barabarani ama kufunga shughuli zao kwa kuwa baadhi ya viongozi wa mamlaka na idara kadhaa za serikali wanapita; ama wakienda kazini asubuhi, ama kurudi nyumbani jioni au pengine kwenda kuhudhuria shughuli nyingine.

Hawa ni pamoja na magari ya mawaziri, manaibu wao, wakuu wa idara za usalama na wengine ambao wanakuwa wakiongozwa na magari ya Polisi au yale yenye vimulimuli vingi, kuashiria kuna mkubwa anaongozwa.

Hali hii imekuwa kero, siyo

Dar es Salaam tu au kwenye miji mingine mikubwa, bali hata mikoani na wilayani. Kwamba anapopita mkubwa, watu wananyimwa uhuru wao wa kujongea kwenda ama kutoka kwenye shughuli zao za kusaka maisha ya kila siku, kisa kuna mkubwa anapita.

Katiba inaamrisha kila mtu mwenye uwezo wa kufanya kazi, afanye shughuli zake halali bila kubughudhiwa na yeyote, lakini anapozingwa na misafara ya viongozi, hata wale wasiohitaji kuzuia watu kuendelea na shughuli zao, inakuwa kero kubwa na uonevu.

Katika kuzuia watu kusonga, kisa misafara, mbali na kwenda ama kutoka kwenye shughuli zao, pia wapo wagonjwa wanaotumia magari binafsi, ambao nao huzuiwa hata kama wanawasha taa za hadhari kuonyesha wanalazimika kuwahi maeneo mahsusi – ikiwamo hospitali.

Inawezekana Dar es Salaam ndiyo inaongoza kwa kero hiyo, lakini kwanini iwe kwenye jiji hilo tu wakati wakubwa wengi wanatakiwa kuwa makao makuu ya nchi, Dodoma? Kwanini wakati mwingi wakubwa hao wapo kwenye jiji ambalo wakazi wake wanatakiwa kukimbizana na muda kwenye shughuli za kuzalisha mali ili waweze kulipa kodi.

Sisi katika Pambazuko tunaomba wakubwa wetu kuacha kupoteza muda wa wananchi barabarani, kisa wao wanapita. Kama ni lazima sana wao “kuwahi,” basi Polisi washauri wakubwa hao kuchelewa kidogo kutoka nyumbani ama kuwahi kutoka kazini, ili wasilete kero zaidi ya barabarani kwani foleni zilizopo ni adha ya kutosha.



## Jisajili kupata Pambazuko bure

Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

Pia unaweza kujisajili kwa kutumia Email hii: [pambazuko1@protonmail.com](mailto:pambazuko1@protonmail.com) ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

## NUKUU



*Wanaume wengi ni kama majani ambayo huanguka na kupepea bila uamuzi, wakati wengine ni kama nyota, wao hufuata njia iliyowekwa, hakuna upepo unaowafikia na wanabeba sheria na njia yao ndani yao.*  
**Herman Hesse**

### Msimamo wetu kuhusu haki za binadamu

**A**YA ya 12 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977) inatamka kwamba “binadamu wote ni sawa,” kwa maana kwamba, binadamu wote ni tofauti na wanyama baki.

Fundisho hili ndio “Dira ya Utanzania” na halitapitwa na wakati kamwe. Hivyo, ni muhimu kuendelea kukumbushana kuhusu umuhimu wake katika sera, sheria na mipango ya maendeleo ya nchi.

Katiba yetu haitamki “usawa wa baadhi ya binadamu,” bali “usawa wa binadamu wote,” wanaojumuisha watoto, watu wazima, wazee, wajane, wagane, walemavu, wagonjwa, wazazi, wagumba na watu wenye afya bora.

Katiba yetu haitamki “usawa wa watu warefu pekee,” bali “usawa wa binadamu wote,” wanaojumuisha watu wafupi, wembamba, na watu wanene.

Katiba haitamki “usawa wa watu wenye anatomia ya kiume pekee,” bali “usawa wa binadamu wote” wenye anatomia ya kike, wenye jenitalia ya kike na jenitalia ya kiume kwa mpigo (herms), wenye sura ya kiume na jenitalia ya kike (ferms) na watu wenye sura ya kike na jenitalia ya kiume (merms).

Katiba yetu haitamki “usawa wa watu wenye uandrophilia pekee,” bali “usawa wa binadamu wote” wakiwemo watu wenye ugainofilia, uambifilia, uheterofilia, uhomofilia, na watu wenye uhanithi.

Katiba yetu haitamki “usawa wa watumishi wa serikali pekee,” bali “usawa wa binadamu wote” wakiwemo watumishi wa mahakama, watumishi wa Bunge, watumishi wa serikali kuu, watumishi wa serikali za mitaa, na watumishi katika sekta binafsi, wakiwamo wakulima.

Katiba yetu haitamki “usawa wa wanachama wa chama tawala pekee,” bali “usawa wa binadamu wote”

wakiwemo wanachama wa vyama vya upinzani pamoja na raia wote wasiofungamana na chama chochote cha siasa.

Katiba yetu haitamki “usawa wa Wabantu pekee,” bali “usawa wa binadamu wote” wakiwemo Waafrika, Waarabu, Wamarekani, Warusi, Wachina, na Wazungu.

Katiba yetu haitamki “usawa wa Wanyamwezi pekee,” bali “usawa wa binadamu wote” wakiwemo Wangoni, Wahaya, Wahehe, na watu wote kutoka kwenye makabila mengine ya Tanzania.

Katiba yetu haitamki “usawa wa Wakristo pekee,” bali “usawa wa binadamu wote” wakiwemo Waislamu, Wahindu, Wabuda, Wabaha, Wazoroasta, Waprotestanti, Walutheri, Wapentekoste, Mashahidi wa Yehova, Wasabato na dini baki.

Katiba yetu haitamki “usawa wa watu wanaoamini katika uwepo wa Mungu pekee,” yaani wafuasi wa mafundisho yenye mrongo wa tehistika, bali “usawa wa binadamu wote” wakiwemo wafuasi wa mafundisho yenye mrongo wa humanistika, deistika, pantehistika, panentehistika, aganostika, na wafuasi wa mafundisho yenye mrongo wa atehistika.

Aidha, Katiba ya Tanzania haitamki “usawa wa wafuasi wa maadili pekee,” bali “usawa wa binadamu wote” wakiwemo waasi wa maadili kama vile wezi, waongo, wachonganishi, wachoyo, wanafiki, wazinzi, waasherati, wabakaji, watesaji, watekaji, wasagaji na walawiti.

Na huu sasa ndiyo msimamo wa gazeti hili, kwamba halina chembe ya ubaguzi Na haya yaliyopo hapa ni “kikonyo” cha usawa wa binadamu wote kama ambavyo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Tangazo la Umoja wa Mataifa Kuhusu Haki za Binadamu vinashuhudia.-

**Mhariri Mkuu**

## Bila Katiba bora, maendeleo ndoto

Dkt. Bullet Ruhinda

**W**IKI iliyopita, gazeti moja la kila siku lililotoka Septemba 13, lilimmukuu mwanasiasa mkongwe, Paul Kimiti akisema na kulisitiza kwamba “wananchi waelimishwe kuhusu Katiba”.

Kimantiki, mwanasiasa huyo alikuwa akimaanisha kwamba wananchi (wengi?) hawajui Katiba ya nchi yao – Tanzania. Je, ni kweli wananchi hawajui Katiba? Ni kigezo gani kinachooonesha kwamba wananchi wengi hawajui Katiba?

Watanania na watu wenye duniani walishuhudia mchakato wa Katiba mpya (katiba ya Warioba) ambayo hata hivyo ilikwama baada ya wanasiasa kuuteka nyara mchakato ule.

Tulishudia Tume ya Katiba ikizunguka nchi nzima kuratibu na kukusanya maoni ya wananchi katika “ujenzi” wa katiba mpya. Watu waliitikia kwa wingi kila mikutano ya tume ilipopita, wananchi walifanya kile walichotakiwa - yaani kutoa maoni yao ambayo yaliratiwa vyema na hata kupatikana rasimu.

Swali linakuja, je, nani aliuwa mchakatoto ule? Ni wananchi wanaodaiwa kutokuwa na uelewa kuhusu Katiba au ni wanasiasa wanaojidai kuijua Katiba?

Kama wananchi walifanya sehemu yao; yaani kukusanya maoni, utasemaje waelimishwe kuhusu Katiba badala ya wale walioharibu mchakato ule kwa kuyapindisha yale waliyotumwa na wananchi kwa kuweka mambo yao wenyewe?

Swali wanalojiuliza watu wengi, ni kwanini linapoongelewa suala la Katiba (mpya) visingizio vya kukwamisha au kuchelewesha kutoka kwa “wanufaika” wa Katiba iliyopo vinakuwa vingi?

Kimiti alinukuliwa akisema “kila mtu ana hamu ya Katiba mpya, lakini tutumie muda, watu waelewe kitu gani kinahitajika ndani yake, inashangaza kusema kwamba kila mtu anahitaji Katiba mpya wakati ni juzi tu wanasiasa wetu walipiga kelele kwamba “huu ni muda wa maendeleo, siyo wa Katiba!”



Jaji Warioba (Picha - Mwananchi)

Unategemea watu wenye mawazo kama hayo wapende Katiba? Lakini pili, kwamba wananchi waelewe kitu gani kinatakiwa kwenye Katiba, kwani maoni yaliyochukuliwa na Jaji Joseph Warioba yalitoka wapi kama siyo kwa wananchi? Iweje leo hawajui tena kinachohitajika ndani ya katiba wakati walitoka maoni yao?

Tatu, nani huyo anayeamua kwamba mambo fulani ndiyo yanahitajika kwenye Katiba? Siyo wananchi wenyewe wanaotoa yale wanayoona yanafaa? Tunaanzaje kuwaambia kwamba kuna yasiyotakiwa katika Katiba? Nani ametoa hiyo “amri” ya kuamua mapenzi au uamuzi wa Watanania?

Mwalimu Nyerere aliwahi kusema; ili tuendeele tunahitahi watu, ardhi, siasa safi na uongozi bora. Mungu alishatuumba sisi watu, hivyo hakuna shida ya watu maana tupo tele. Mungu pia alitupatia ardhi (na rasilimali zote) hivyo ardhi siyo tatizo maana ipo tele. Tatizo lipo kwenye uongozi bora na siasa safi, ili viwili hivyo viweze kuongoza watu kutumia rasilimali kuleta maendeleo.

Lakini siasa safi na uongozi bora havina budi kutokana na Katiba bora. Bila mwongozo thabiti ambao umo katika Katiba bora, maendeleo tutaendelea kuyasikia! Hivi sasa Katiba yetu ina ‘mashimo’ mengi mno yanayoweka vizingiti vikubwa kwa maendeleo yenye kudumu kwa vizazi na vizazi.

### Wageni 1000 kumzika Malkia leo



**W**AKUU wa nchi ambazo zimekuwa na mvutano na Uingereza katika kutekeleza sera za nje, biashara na hata masuala ya amani, ni miongoni mwa waalikwa katika maziko ya Malkia Elizabeth II yanayofanyika leo.

Mataifa yaliyoingia kwenye mgogoro wa kidiplomasia na Uingereza kwa nyakati tofauti, lakini yamepata mwaliko ni China, Iran, Nchi za Falme za Kiarabu,

Malkia Elizabeth II (96) alifariki dunia Septemba 8, 2022, atazikwa leo – Septemba 19, ndani ya Kanisa Kuu la Kumbukumbu ya Mfame George VI, eneo la Windsor kaskazini mwa Jiji la London.

Mataifa sita yaliyonyimwa kabisa mwaliko kwenda kumzika Malkia ni pamoja na Russia, Venezuela, Beralus, Afghanistan, Syria na Myanmar. Mataifa haya yanatajwa na Uingereza kukiuka haki za binadamu, ikiwamo kuua na kuminya uhuru wa vyombo vya habari.

Rais wa Marekani, Joe Biden ataongoza wakuu wote walioalikwa na kwamba kusanyiko hilo linaelezwa kuwa kubwa zaidi kutokea baada ya miongo kadhaa kupita. Inaelezwa kuwa hilo ni kusanyiko kubwa kutokea baada ya mwaka 1965 wakati Waziri Mkuu wa Uingereza Winston Churchill anazikwa.

*London (Mashirika)*

### ‘Bwana Mchungaji Wangu’ kuimbwa

**W**IMBO maarufu wa ‘Bwana Ndiye Mchungaji Wangu’ ulioko katika vitabu vingi vya nyimbo ya Kikristo, ndiyo utapamba maziko ya Malkia Elizabeth II wa Uingereza yanayofanyika leo.

Inaelezwa kwamba wakati wa uhai wake, Malkia huyo alikuwa mpenzi wa wimbo huo na kwamba haikupita siku bila kuuimba. Utaimbwa na kwaya ya kanisa anamozikiwa.

Baadhi ya nota za wimbo huo ni: Bwana ndiye mchungaji wangu, sitapungukiwa na kitu, katika malisho ya majani mabichi hunilaza kando ya maji ya utulivu huniongoza.

Unaendelea; Hunihuisa nafsi yangu, na kuniongoza, katika njia za haki kwa ajili ya jina lake nijapopita kati ya bonde la uvuli wa mauti, sitaogopa mabaya.

*London (CM)*

### Aliyetabiri kifo cha Malkia Twitter afungwiwa

**M**CHANGIAJI mmoja katika Twitter, Makijiita Logan Smith, amefungwiwa na mtandao huo baada ya kubainika ‘alitetabiri’ kifo cha Malkia wa Uingereza, Elizabeth.

Logan aliandika katika ukurasa wake, Juni 7, 2022 kwamba Malkia atafariki dunia Septemba 8, mwaka huu. Kifo cha kiongozi huyo wa Uingereza kilitokea tarehe hiyohiyo.

Mbali na kutabiri hivyo, Logan pia ametabiri kifo cha mrithi wa Malkia Elizabeth, Mfalme Charles III kwamba kitakuwa Machi 28, 2026.

*London (Mtandao)*

## Ruto aanza kwa mguu mbaya

Na Mwandishi WETU, Nairobi

“NAOMBA kabisa mashirika na taasisi za serikali zisitumie pesa za walipa kodi kwa kuweka matangazo ya kunipongeza magazetini. Twendeni tukachape kazi kwa ajili ya Wakenya na kupigania maendeleo ya nchi yetu.”

“Hawa rafiki zangu wa Citizen wako wapi? Mbona siwaoni hapi? Hebu tujipange kufanya kazi.”

Hizi ni kauli za Rais wa Kenya, Dkt. William Ruto baada ya kuanza majukumu yake akiwa ni kiongozi mkuu wa nchi hiyo ya Afrika Mashariki.

Kauli mbili za Ruto; ya kwanza inabeba maana kwamba vyombo vya habari, vikose mapato halali, hivyo huenda anataka kuviziba pumzi ya mapato ili vife na – ya pili ikionyesha kejeli kwa kituo cha televisheni cha Citizen ambacho kilimpa nafasi finyu wakati wa kampeni zake.

Ruto alitangazwa kuwa mshindi dhidi ya mpinzani wake mkubwa, Raila Odinga katika Uchaguzi Mkuu wa Kenya uliofanyika Agosti 9. Odinga alikwenda mahakamani kupinga ushindi huo ambako nako ‘aliangukia pua.’

Kabla na wakati wa kampeni za uchaguzi huo, hasa kwa ngazi za urais, magazeti makubwa ya Kenya, hayakutoa nafasi sawa kwa wagombea wakubwa; Raila na Ruto. Kulikuwa na ushahidi wa dhahiri kwamba vyumba vya habari vya kampuni ya Nation na The Standard, vyote vilionekana kumpendelea Raila na kumpa nafasi kubwa zaidi ya kuibuka mshindi.

Hataua ya vyombo hivyo ililalamikiwa na timu ya kampeni ya Ruto mara kwa mara, lakini vyombo hivyo viliziba masikio na kuendelea kumpa nafasi na muda mrefu Raila.

Wachambuzi wa siasa na wale wa maudhui ya vyombo vya habari wameeleza kuwa magazeti makubwa, vituo vya televisheni vinavyoaminika, vilimpa upendeleo Raila kwa kuamini kuwa atashinda uchaguzi huo.



Rais William Ruto

Sababu kubwa ya imani yao ikiwa ni kupigiwa chapuo na hata kampeni na Rais Uhuru Kenyatta ambaye amemaliza muda wake wa urais tangu Septemba 13, baada ya Ruto kuapishwa.

Inaelezwa pia kwamba vyombo hivyo vikubwa vya habari viliendesha kampeni ya siri ya kupaza sauti kwamba “lazima” Raila, maarufu kwa jina la Baba, ashinde na kushadadia matokeo ya kura za maoni ambazo ziliendeshwa na wao au kampuni binafsi.

Wachambuzi wa habari na siasa za Kenya wanaeleza kuwa kutokana na mazingira haya, na baada ya Ruto kuanza kazi akiwa ni rais wa tano wa Jamhuri ya Kenya, huenda vyombo vya habari vikaanza kusakamwa na mamlaka na hata baadhi ya wakala wa serikali ili kuviminya na kupunguza mapato yao kutoka kwenye matangazo ya mawakala, mashirika na hata kampuni zinazosimamiwa na serikali.

Pamoja na ukwepo sheria kadhaa zinazolinda uhuru wa habari na mawasiliano nchini Kenya, bado rais akiamua “kusumbua” vyombo vya habari, anaweza.



### Umiliki wa taifa – I

**Na Askofu Dkt. Stephen MUNGA**

**K**ATIKA makala yaliyopita tuliangalia Namna taifa linavyoweza kuundwa. Tuliangalia kwa kifupi juu ya “uwiano wa matarajio katika kuundwa kanuni” kama kigezo cha msingi ambacho huturejesha kwenye wazo la “nafasi ya asili” ikiwa ni mchakato wa kutunza uwiano huo wa matarajio katika kuundwa kanuni.

Haya yanakazia nia madhubuti ya kuunda siasa safi. Wazo la siasa safi huleta uelewa wa ulinganifu (relative meaning) kwa maana ya kwamba yawezekana kuwa na tofauti za viwango vya upimaji wa siasa safi kulingana na muundo wa uumbaji wa siasa zenyewe.


Nimeweka mkazo katika jamii kama muundo wa msingi kwenye kuundwa taifa. Miundo tofauti ya jamii imekuwa katika mijadala ya nyakati hizi katika falsafa ya siasa kwa kipindi kirefu na nina hakika itabaki hivyo kwa kipindi kirefu kijacho.

Hii imetokana na dhana kwamba mambo makubwa yanayogusa maisha ya watu yanategemea jinsi gani yafuatayo yanaguswa na siasa - uhuru na ustawi wao, hamu, matakwa yao, nafasi ya kuonyesha uwezo wao, na kutimizwa kwa mahitaji yao. Kwa sehemu haya ndio hufunua maana ya uwiano wa matarajio katika kuundwa kanuni na kuongoza jamii.

Tulitaja kwa kupitia kubuniwa serikali katika mihimili mikuu mitatu. Kwa lugha rahisi kusudi la mihimili hiyo ni kuhifadhi na kuboresha uwiano wa matarajio na kuuboresha kwa kurejea mara kwa mara kwenye “nafasi ya asili”.

Haya yanafanyika kwa imani kwamba taifa lina watu wa aina ile tuliyojadili tulipojadili “watu.” Hawa ni watu ambao hawapo kwa ajili ya kujali matumbo yao na faida binafsi.

Watu watumiao fursa zao kuumiza watu wengine ni sawa na kuwachukulia kama wamejiangua na jamii ambayo



*Mwl. Nyerere- Muumini mkubwa wa siasa safi*

nimeitaja kuwa msingi wa kuundwa taifa.

“Uwiano wa matarajio” katika kuundwa na kusimamia utekelezaji wa kanuni zilizotungwa kwa manufaa ya jamii ni kigezo muhimu cha kuzingatwa. Pasipo kuwa na watu wanaotazama na kueleweka hivyo (wenye nia hiyo) taifa litaishi kwenye kuunda kanuni za wanaojipendelea na kunufaisha wale wanaozitunga.

Nadhani karaha nzima ya “tozo” inayorindima katika taifa letu ni matokeo ya watengeneza na wasimamizi wa kanuni wasio na kipimo sahihi cha kutunza “uwiano wa matarajio” ya jamii wanayoitawala.

Maelezo haya ni sehemu ya siasa ambayo bado inazo nyuzi nyingi zinazoning’inia ambazo hazijaunganishwa pamoja. Bado hata sijazungumza juu ya mihimili ya serikali na nafasi zao katika kuunda na kuhifadhi siasa safi kwa misingi ya mawazo niliyoyaeleza mpaka hapa.

Nitaendelea kuunganisha nyuzi hizo polepole hadi tutakapoelewana.

---





Na Evarist Chahali  
evarist@chahali.com

## Ujengwe utamaduni kuomba radhi

**L**EO ni siku ya mazishi ya Malkia Elizabeth II aliyefariki Septemba 8, 2022. Mazishi hayo yanahitimisha siku 10 za maombolezo ya kitaifa nchini Uingereza. Atazikwa katika Kanisa la Mtakatifu George lililopo kwenye moja ya makazi yake, boma la Windsor.

Zaidi ya wageni 500 wanaojumuisha viongozi wa nchi, ikiwa ni pamoja na Rais Samia Suluhu Hassan, na watu wengine maarufu duniani, watahudhuria mazishi hayo.

Kama nilivyogusia kwenye safu hii katika toleo la wiki iliyopita la gazeti hili, japo idadi kubwa ya watu hapa Uingereza na duniani kwa ujumla imegubikwa na majonzi kufuatia kifo cha Malkia huyo, kuna watu mbalimbali ambao siyo tu wanamhusisha kiongozi huyo na maovu ya dola ya Uingereza ikiwa ni pamoja na ukoloni, bali pia wanasikitishwa na ukweli kwamba hakuwahi kuomba radhi kwa maovu hayo.

Ingawa kuomba radhi hakufuti “mabaya” yaliyotokea huko nyuma, kwa kiasi fulani huleta faraja kutokana na wahusika kukiri “makosa” yao.

Utaratibu kama huo umekuwa na ufanisi mkubwa huko Afrika Kusini baada ya kuisha kwa mfumo wa ukaburu.

Kwa bahati mbaya, kwa Tanzania yetu, hakuna utamaduni wa watawala kuomba radhi. Kwa mfano, licha ya baadhi ya hatua zilizochukuliwa katika utekelezaji wa Azimio la Arusha ziliwaathiri baadhi ya wananchi wasio na hatia, watawala hawakuomba radhi.

Kadhalika, watawala hawajaomba radhi kufuatia mauaji yaliyotokea huko Zanzibar mwaka 2001 kufuatia vurugu za uchaguzi mkuu wa mwaka 2000.

Lakini pengine kubwa zaidi ni yaliyojiri katika utawala uliopita kabla ya ujio wa Rais Samia. Ni “siri ya wazi” kwamba



Malkia Elizabeth wa Pili

kulikuwa na ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Kuna Watanania waliotekwa, walioteswa, walionyang’anywa mali zao, na baadhi walipotewa uhai.

Mwanahabari mmoja alitupwa jela kwa takriban miezi 10, na alipoachiwa huru, alitakiwa kulipa zaidi ya shilingi milioni 100 kwa makosa ambayo sasa yamebainika kuwa ni feki ya utakatishaji fedha na uhujumu uchumi.

Kiongozi mmoja wa Mkoa wa Dar es Salaam ambaye alihusishwa na matukio mbalimbali yaliyojiri zama hizo, akiwa madarakani, hadi sasa hajachukuliwa hatua kutokana na maovu aliyotenda.

Japo watawala hawawezi kukwepa lawama kwa kupuuzia umuhimu wa kuomba radhi kwa wahanga wa ukiukwaji mbalimbali wa haki zao, wahanga hao nao wanaweza kubeba lawama kwa kutofanya jitihada za kudai waombwa radhi.

Japo yaliyopita siyo ndwele, samahani haigombi.

---

# Tumuombee Lowassa

Na Mwandishi WETU

**H**ISTORIA ya ukombozi wa elimu ya Tanzania, hasa kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Dodoma, kuwepo kwa shule za sekondari za kata na mtandao wa maji kutoka Ziwa Victoria hadi Kahama, kamwe haiwezi kuelezwa bila kutajwa kwa jina la Edward Ngoyai Lowassa.

Hayo ni mafanikio machache makubwa kati ya mengi aliyواسisi Lowassa wakati wa utumishi wake katika Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ngazi mbalimbali, hasa akiwa waziri mkuu kwa miaka mitatu; 2005 hadi 2008.

Lowassa ambaye alikuwa miongoni mwa viongozi wanaopamba vichwa vingi vya habari katika magazeti, redio na televisheni, sasa hajaonekana kwa muda mrefu, huku Watanzania wakiuliza “yuko wapi mpendwa wao?”

Gazeti la Pambazuko limeelezwa kuwa Lowassa ni mgonjwa na kwamba yuko nchini Afrika Kusini ambako anapatiwa matibabu baada ya kukumbwa na changamoto ya afya.

Hata hivyo, mmoja wa familia yake pamoja na kukiri Lowassa kuwa nje ya nchi kwa matibabu, lakini haikuwa tayari kueleza anakoendelea kupata tiba kiongozi huyo aliyewahi kutikisa anga za siasa kwa utendaji wake akiwa serikalini.

Pamoja na familia kukiri kwamba Lowassa anaendelea na matibabu nje ya nchi, lakini inaelezwa kuwa afya kwa sasa ina nafuu, ingawa hali imekuwa ikibadilikabadilika.

“Naomba tuendelee kumuomba mzee wetu, anumwa, lakini nikuhakikishieni kwamba afya yake imekuwa ikiimarika, ingawa anahitaji kuendelea kuwepo kwenye uangalizi maalum wa madaktari na wauguzi,” anasema mwanafamilia huyo ambaye hakutaka kutaja jina lake gazetini.

Pambazuko limefanya jitihada za kufahamu yuko mji gani ama hospitali anayotibiwa, lakini limeombwa na familia



Edward Ngoyai Lowassa.

kutotaja mji anakoendelea na matibabu na uangalizi wa wataalamu wa afya.

Maadili na sera ya gazeti la Pambazuko yanakataza kueleza kwa undani changamoto ya afya anayokabiliwa nayo Lowassa, kama ilivyo kwa mtu yeyote, labda kwa matakwa yake.

Mwanafamilia huyo anaeleza kwamba Lowassa anahitaji zaidi maombi ya Watanzania ambao anaeleza kuwa “anawapenda sana,” na anatamani apone haraka ili kurejea nchini kwake kwa ajili ya kushiriki mapambano ya kuuondoa umasikini.

Lowassa wakati akiwa waziri mkuu alikuwa akieleza vipaumbele vyake vitatu kuwa ni; “elimu, elimu na elimu,” msimamo ambao ulimsukuma kushadadia na kusimamia kwa nguvu kuanzishwa kwa Chuo Kikuu cha Dodoma na kuwepo kwa shule za elimu ya sekondari kila kata.

Mbali ya kuanzishwa kwa chuo kikuu, shule za sekondari za kata, Lowassa pia alihakikisha wananchi wa maeneo ya mikoja ya Mwanza, Shinyanga wanapata maji kutoka Ziwa Victoria.

Taarifa zinaeleza kuwa Lowassa alishauriana na timu ya wataalamu wakati akiwa wizara ya maji na kukubali wazo lake la kuwepo uwezekano wa

## Tumuombe Lowassa

kuvuna maji ya Ziwa Victoria kwa ajili ya matumizi ya majumbani na hata viwandani, lakini alipowasilisha wazo hili kwenye baraza la mawaziri, chini ya Rais Benjamin Mkapa, sehemu kubwa ya baraza ilingomea na kumwambia kwamba “haiwezekani.”

Hata hivyo, katika moja ya maelezo yake, Lowassa alimtaja Jakaya Kikwete, wakati huo akiwa waziri wa mambo ya nje, alikubali na kuunga mkono wazo lake. Pia aliyemuunga mkono ni Mohamed Seif Khatibu, aliyekuwa Waziri wa Nchi katika Ofisi ya Makamu wa Rais. Khatibu sasa ni marehemu.

“Niwapeni siri, nilipendekeza mradi wa kutumia maji ya Ziwa Victoria kwa Rais Mkapa ambaye akaniuliza wale wakubwa tutawaweza, nikamhakikishia tutawaweza. Wakubwa hao alikuwa na maana ya nchi za Misri, Ethiopia na Sudan zinazotumia Mto Nile unaoanzia kwenye Ziwa Victoria. Mzee Mkapa baada ya kusikiliza mawazo yote akaamua fedha zitolewe,” alisema Lowassa.

Lowassa kabla ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, aliondoka Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kujiunga na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) ambako alipitishwa kugombea nafasi ya urais katika uchaguzi mwaka huo, hata hivyo, Tume ya Uchaguzi (NEC) ilimtangaza mgombea wa CCM, John Magfuli kuwa mshindi.

Kabla ya kujiondoa CCM, Edward Lowassa alikuwa mwanachama wa CCM kwa muda wa miaka 38, ambapo alijiunga na chama hicho mara tu baada ya kumaliza elimu yake ya chuo kikuu mwaka 1977. Hata hivyo, baadaye – Machi Mosi, 2019, Lowassa alirejea CCM.

Hatawa ya mwanasiasa huyo mashuhuri nchini Tanzania kuamua kujiunga na chama cha upinzani Chadema, ikiwa imebaki miezi mitatu tu kuelekea uchaguzi mkuu, ilibadilisha kabisa upepo wa kisiasa nchini Tanzania.

Lowassa alijiuzulu wadhifa wa

waziri mkuu kufuatia kashfa ya rushwa iliyohusisha kampuni ya kuzalisha umeme ya Marekani - Richmond Development Company LLC ya jiji la Houston, Texas.

Hata hivyo wakati anatangaza kuhamia kwake Chadema, Lowassa alikanusha katu kuhusika kwa namna yoyote na kashfa hiyo na kudai kuwa yeye alifuata tu amri kutoka kwa ‘wakubwa’ walio juu yake.

“Kama kuna mtu yeyote mwenye ushahidi basi na aende mahakamani ama sivyo anyamaze” alisema Lowassa.

Kuhama kwake kunamfanya Lowassa kuwa ndie kiongozi wa kwanza wa ngazi ya juu kabisa wa CCM kukihama chama hicho tangu kuanza kwa mfumo wa vyama vingi nchini Tanzania mnamo mwaka 1992.

Mwanajeshi huyo wa zamani na aliyewahi kupigana wakati wa vita kati ya Uganda na Tanzania mwaka 1978 -79, Lowassa aliiambia hadhara kwamba akiwa mtu mwenye uchungu na nchi yake, isingekuwa rahisi kubaki ndani ya CCM huku akiona chama hicho kimepoteza mwelekeo na sifa ya kuongoza nchi.

Wakati wa mchakato wa ndani wa cha CCM kumpata mgombea urais, Lowassa alipata wadhamini 700, 000, tofauti na idadi iliyokuwa ikitakiwa ya kuwa na saina za wadhamini 450.

Hata hivyo mchujo wa chama ulipofanyika jina lake lilikatwa mapema kabla hata ya kupelekwa kwenye vikao vya vya juu vya chama hicho. Ambapo baadaye waziri wa ujenzi. Wakati huo, John Pombe Magfuli ndiye aliyeibuka kidedea na kuwa mgombea kupitia chama hicho tawala.

Mbali na maji na shule za kata, Lowassa anabaki katika historia kuwa ni waziri mkuu mwenye uamuzi mgumu, kama ilivyokuwa kwa Edwaezi Sokoine na kwamba jitihada nyingine kubwa la Lowassa ni kubwa na mafanikio ya upatikanaji wa fedha za kujenga chuo kikuu cha Dodoma.

### Wamjaribu Rais Mwinyi

Na Mwandishi MAALUM

**W**AFANYABIASHARA kutoka Dubai, huenda wakakwama kupata eneo la kuwekeza kama walivyoahidiwa na Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Hofu hiyo inafuatia kuwepo eneo aliloelezwa Rais Mwinyi kwamba lipo tayari kwa ajili ya uwekezaji, lakini kumbe baadhi ya watendaji serikalini hawakueleza kuwepo kwa mwekezaji mwingine.

“Hatua hii ya kutomweleza ukweli Rais Mwinyi kuhusu eneo hilo, ni kama kumcheza simba sharubu, lazima atachukua hatua kali dhidi yao,” amedokeza mmoja wa maofisa wa Ikulu ya Zanzibar ambaye alibaini udanganyifu huo

Taarifa ambazo Pambazuko imeelezwa ni kwamba uamuzi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kusitisha Hatimiliki ya ardhi katika eneo la zaidi hekta 400 sasa, ni njia ya kumuhadaa Rais Mwinyi ili kupewa wawekezaji tarajali kutoka Dubai.

Tayari wamiliki wa eneo hilo wamejieleza katika sauti ya kulalamika kwamba wanaishangaa serikali kuibuka sasa na kudai eneo hilo linapokwa hatimiliki wakati walimilikishwa kihalali na kwamba wanaendelea kulitumia.

Pennyroyal Limited (Zanzibar) ndiyo kampuni wamiliki wa ardhi hiyo ambayo sasa serikali imeinyakua kwa kisingizio cha kuwepo mgogoro. Kampuni hiyo ilipewa ardhi hiyo kwa hatimiliki kwa miaka 99.

Hata hivyo, Pambazuko imebaini kwamba katika sehemu ya eneo hilo, kuna mgogoro wa viwanja viwili; Na. 1107 na Na. 1118 katika eneo la hekta 411 zilizokodishwa na mwekezaji huyo.

Uisitishaji hatimiliki ya ardhi unafanywa wakati Pennyroyal inaendelea kukamilisha miradi kwenye eneo hilo ikiwamo hoteli za nyota tano; kiwanja cha kucheza gofu na eneo la burudani



Rais Mwinyi

za boti za kifahari (yatch) na nyumba za kuishi.

Brian Thomson, Mkurugenzi Mtendaji wa Pennyroyal, anasema; “tumejitahidi kuhakikisha mradi huu hauporomoki. Jitihada zetu zimeambulia patupu kwani serikali sasa imekamia kutunyang’anya ardhi.”

Wakati wa ziara ya Rais Mwinyi hivi karibuni huko Uarabuni alikutana na wafanyabiashara na kuwaomba kuwekeza Zanzibar ambako aliahidi kuwapa eneo la kufanya uwekezaji wao.

Ofisa mmoja katika Pennyroyal amedai “maelezo ya kina” yalipelekwa kwa Rais Mwinyi kujulishwa kuwa panapokusudiwa kuchukuliwa kwa ajili ya matumizi mengine, kuna shughuli za uwekezaji zinaendelea, ambako kuna miradi inayohusisha wawekezaji washirika.

“Yawezekana watendaji wamejiingiza kwa maslahi binafsi huku wakisingizia kutekeleza maelekezo ya wakubwa wao,” anasema ofisa mwingine wa kampuni hiyo.

Mudrick Soraga, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji, amesema; “tumefungwa mikono. Suala hili analishughulikia Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

## Neema bima ya afya yasubiriwa

Na Tryruckia MFINANGA

**A**KIHUTUBIA Watanzania kupitia sherehe za kutimiza miaka 50 ya chama cha kitume cha Wanawake Katoliki Tanzania (Wawata), uliofanyika kwenye Uwanja wa Taifa, jijini Dar es Salaam, Septemba 10, 2022, Rais Samia Suluhu Hassan alilitangazia taifa kwamba Bunge la Septemba, mwaka huu litapokea, kujadili na kupitisha muswada wa Bima ya Afya kwa Watanzania Wote.

Tangazo hili linamaanisha kwamba sasa juhudi za taifa hili kupiga vita ujinga, maradhi, umaskini na ubaguzi, kwa kukuza huduma za kijamii katika sekta ya elimu, afya, uchumi, zitakuwa 'zimepigwa jeki' kwa kiwango kinachogusa maisha ya kila mwananchi, lakini kupitia sekta ya afya.

Utafiti unaonyesha kuwa sasa, sekta ya afya, nchini Tanzania, inazo sifa zifuatazo; huduma duni za kiafya, upungufu wa dawa na vifaa tiba, mishahara midogo, mazingira duni ya kazi, utoaji wa huduma za kiafya kwa watu wanaotoka kwenye kaya maskini, na kuna wagonjwa wasioweza kulipia huduma za kiafya kwa kutumia fedha taslimu.

Wachambuzi wa masuala ya huduma za afya wanasema kuwa, mifuko ya bima ya afya ni mbinu mojawapo ya kutatua baadhi ya changamoto hizi.

Imebainika kuwa kwa sasa, sekta ya bima ya afya nchini inayo mifuko mitano. Kwa pamoja, mifuko hii inahudumia asilia 16.1 ya Watanzania wote.

Mifuko hiyo ni Mfuko wa Bima ya Jamii (CHF) au Tiba Kwanza Kadi (TIKA), unaohudumia asilimia 8.4 ya wagonjwa wote; na Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), unaohudumia asilimia 5.6 ya wagonjwa wote.

Pia kuna Mfuko wa Mafao ya Afya ya Jamii (SHIB), unaohudumia asilimia 0.1 ya wagonjwa watu wote, huduma zake zikipatikana kupitia Mfuko wa Pensheni wa Taifa (NFFS); Mfuko wa Bima Binafsi



Wasiri wa Afya, Ummu Mwalimu

ya Afya (PHI), unaohudumia asilimia 1.0 ya wagonjwa watu wote.


Mbali na mifuko iliyotajwa hapo juu, pia kuna Mfuko wa Bima ya Afya Unaochangiwa na Wananchi (CHI), unaohudumia asilimia 1.0 ya wagonjwa wote.

Takwimu hizi maana yake ni kwamba kati ya Watanzania wanaokadiriwa kufikia milioni 55, ni Watanzania 8,855,000 pekee wanaopata huduma za kiafya kwa kutumia huduma za bima ya afya. Hivyo, asilimia 83.9 ya Watanzania, sawa na watu 46,145,000, wanalazimika kupata huduma za afya kwa kugusa mfukoni.

Na kama mtu hana akiba ya matibabu, basi anahamia kwenye miti shamba. Kama miti shamba isipokuwa na msaada, basi husubiri kifo. Hivyo, juhudi za serikali ya Rais Samia kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya kwa Watanzania Wote zimekuja katika wakati muafaka.

Pamoja na kuwa Rais Samia hakutaja bajeti ya mfuko alioutangaza, basi hakusema kila Mtanzania ametengewa shilingi ngapi, bado imani ya wananchi ni kuwa afya zao sasa huenda zikalindwa zaidi na zaidi kwa uhakika wa tiba.

### Tutakumbuka Daima...



*Kwamba muasisi wa Tanzania, Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, aliamini katika mawazo shirikishi. Katika uongozi wake, aliwapa nafasi wasaidizi wake kueleza mawazo yao juu ya mambo kadhaa ya nchi na aliwasikiliza. Hapa anaonekana akiwa na Samuel Malecela, ambaye aliwahi kufanya naye kazi kwa karibu. Baadaye Malecela alipata kuwa waziri mkuu. Mwalimu sasa ni marehemu. (Picha ya Maktaba ya Pambazuko).*

---



## Njeo katika kitenzi



## Na Dkt. Michael Mashauri

**K**ISWAHILI ni miongoni mwa lugha zinazokua kwa kasi kubwa kila siku duniani. Vyuo vikuu nje ya Afrika, vimeanza kufunza lugha hiyo adhimu. Kutokana na umuhimu wake, Pambazuko limeamua – kila wiki, kuwa njia ya kufundisha Kiswahili bure kwa yeyote anayependa.

Katika Kiswahili kuna hali ya mazoea na timilifu. (There are habitual and perfect aspects in Kiswahili).

## Hali ya Mazoea (Habitual tense)

Hali ya mazoea katika Kiswahili hutambulishwa na kiambishi HU- kinachojitokeza kabla ya mzizi. Kinapotumika, kitenzi hudondosha viambishi vingine vikiwemo vya nafsi na njeo katika uyakinishi. Kiambishi hiki kinaweza kuambatana na maneno kama kila saa/siku/asubuhi/jioni/wiki/mwezi/mwaka, mara kwa mara baada ya kitenzi. (Habitual tense in Kiswahili is introduced by the prefix **HU-** which appears before the verb root. When using it, the verb drops other prefixes including personal and tense prefixes in affirmation. It can also be accompanied by words like *every hour/day/morning/evening/week/month, often after the verb*).

## Examples

Mimi **hupenda** wali (I like rice)

Wewe **hula** sana kila asubuhi (You eat too much every morning)

Yeye **huingalia** mpira wa miguu mara kwa mara. (He/she often watches football match)

## A. Hali timilifu (Perfect tense)

Hali timilifu huonyeshwa kwa kiambishi -ME- katika uyakinishi ambacho hujitokeza baada ya kiambishi cha nafsi na kuafuatiwa na mzizi. Kwa upande wa vitenzi vya silabi moja hufuatiwa na -KU-. Katika hali ya kuonyesha msisitizo, huweza kufuatiwa na -SHA- na kuwa -MESH- ikiwa na maana ya 'tayari'. Hali timilifu huonyesha ukamilifu wa tendo ndani ya muda mfupi uliopita na matokeo ya ukamilifu wake bado yapo. (Perfect tense is shown by the prefix -ME- in affirmative state which comes after personal prefix and before the root of the verb. In monosyllabic verbs it is followed by -KU-. When showing insistence, it can be followed by -SHA- and become -MESH- to mean 'Already'. This tense shows completion of an action in the immediate past and the effects of its completion is still experienced).

## Examples

Mimi **nimekula** ndizi (I have eaten banana)

Wewe **umeogea** sana (You have talked too much)

Yeye **ameshaondoka** (He/she has left already)

• **Mwandishi wa Darasa la Kiswahili ni Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.**



### Eacop yajali viwango, EU hawana taarifa sahihi



Bomba la mafuta

#### Na mwandishi WETU

**U**PPO uwezekano mkubwa kwamba Bunge la Umoja wa Ulaya (EU) halina taarifa sahihi kuhusu Mradi wa Bomba la Kusafirisha Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (Eacop).

Kutokana na kupata taarifa zisizokuwa na ukweli, ndiyo maana limetoa tamko kulaani uvunjifu wa haki za binadamu na kile wanachoeleza kuwa ni uharibifu wa mazingira unaodaiwa kufanywa na mradi wa Eacop unaotekelezwa nchini Uganda na Tanzania.

Bunge hilo, lililokutana Agosti 14, 2022 mjini Strasbourg, Ufaransa, linahimiza kwamba utekelezaji wa mradi huo ucheleweshwe angalau kwa mwaka mmoja ili kuweka mazingira yaliyo rafiki na kutekelezwa kwa matakwa ya haki za binadamu.

Ikulu ya Uganda, bunge la nchi hiyo na serikali ya Tanzania zimejitokeza kujibu na kueleza ukweli wa hali halisi inayolalamikiwa na bunge hilo linalojumuisha nchi 27 zikiwamo nchi tajiri za Bara la Ulaya.

Bunge hilo lilieleza kuwa Novemba 9, 2021, timu ya waangalizi wa kimataifa kutoka balozi za Ufaransa, Ubelgiji, Denmark, Norway na Uholanzi, walikosa fursa ya kuingia kwenye eneo la mradi wa mafuta na gesi nchini Uganda, kitendo ambacho kinaelezwa hakikuwa sawa. Hata hivyo, inaelezwa kuwa wajumbe

hao walienda kwenye eneo ambalo halikuwa na taarifaza ujio wao.

Pia bunge hilo linadai kuwepo kwa watu wapatao 100,000 wanaokabiliwa na tishio la kuhamishwa kinyemela ili kupisha mradi wa Eacop, kabla hatua stahiki za kuwafidia kukamilika.

Serikali za Uganda na Tanzania, kwa kutumia takwimu zinaeleza kuwa watu wanaoguswa na ujenzi wa mradi huo mkubwa wanafikia 10,000 na kwamba wote watapokea stahiki zao kabla ya kuondoshwa kwenye maeneo yao.

Ukweli unaolelezwa na Eacop na nchi na kampuni wahuusika ni kwamba watu wanaoguswa na mradi huo, wananufaika kwa nyumba za kisasa, mashamba, chakula kwa mwaka mzima au zaidi, kupewa elimu ya biashara na zaidi sana fidia ambayo wanashauriwa namna ya kuituimia vyema.

Tayari Rais wa Uganda, Yoweri Museveni amelijibu Bunge la Ulaya na dunia kwamba mradi huo utaendelea kwa kuwa hauharibu maisha ya binadamu na hata wanyama.

Katika taarifa yake iliyotolewa Ijumaa iliyopita, Rais Museven alisema wananchi wa Uganda wasiwe na wasiwasi na msimamo wa nchi za Ulaya kuhusu kusitishwa kwa maendeleo ya mradi huo wa bomba la mafuta, kwani mafuta yataanza kutoka kama ilivyopangwa – mwaka 2025.

## **Eacop yajali viwango, EU hawana taarifa sahihi**

Akiungana na Rais Museveni, Naibu Spika wa Uganda, Thomas Tayebwa, aliliambia Bunge la Ulaya kwamba, mradi wa Eacop uliidhinishwa na Bunge la Uganda, ambacho ni chombo cha nchi huru, na kwamba, hatua yoyote ya Bunge la Ulaya kukosoa uamuzi wa Bunge la Uganda ni shambulio dhidi ya uhuru wa Bunge la Uganda ambayo ni nchi huru.

Bunge la Uganda limelitaja tamko la Bunge la Ulaya kama mkakati wa ubaguzi wa kiuchumi, naolenga kuwanyima watu wa Afrika Mashariki fursa kutoka kwenye sekta ya mafuta na gesi.

Kuhusu madai kwamba, mradi wa Eacop utaharibu mazingira, Bunge la Uganda limewashangaa wenzao wa Bunge la Ulaya, kwani Ulaya yenye asilimia 10 ya watu wote duniani huchangia asilimia 25 ya gesi ya ukaa, wakati Afrika yenye asilimia 20 ya watu wote duniani huchangia asilimia tatu pekee ya gesi ya ukaa.

“Kihistoria, Umoja wa Ulaya na nchi nyingine za Magharibi ndio chanzo kikubwa cha mabadiliko ya tabianchi,” alisema Naibu Spika wa Uganda, Thomas Tayebwa.

Kisha, Tayebwa akamalizia kwa kuuliza swali lifuatalo: “Kama hivyo ndivyo, nani anapaswa kusitisha au kupunguza kasi ya kuharibu mazingira?” Jawabu la Tayebwa likawa kwamba, “Bila shaka siyo Afrika wala Uganda, bali Ulaya.”

Nayo serikali ya Tanzania imesema hakutakuwa na athari zozote za kimazingira wakati wa utekelezaji wa mradi huu kwani tahadhari zote zilizingatiwa kitalaamu. Waziri wa Nishati, Januari Makamba alitoa kauli hiyo wiki iliyopita - Septemba 16, 2022 akiwa anajibu tamko la Bunge la Ulaya (EU).

Makamba alisema kwamba, hakuna ardhi itakayochukuliwa na mradi bila kufanyiwa fidia. Makadirio yanaonyesha kwamba, fidia itafika kiasi cha bilioni 23 za Tanzania kwa wakazi 9,122.

Katika tovuti ya Eacop, inaeleza kwamba utwaaji ardhi unazingatia sheria

zote mbili za Tanzania na Viwango vya Utendaji vya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF).

Inaelezwa kuwa kwa upande wa Tanzania, wapo watu 9,513 wanaoguswa na mradi huo ambao wote watalipwa fidia stahiki kwa ardhi, mazaao, nyumba na mali zingine wanazomiliki.

Katika waguswa hao, wapo pia waliochagua, kwa hiari yao kujengewa nyumba na kupewa mashamba yenye ukubwa wa ardhi waliyokutwa wakiimiliki.

Mradi wa Eacop unatekelezwa kwa ushirikiano wa serikali za Uganda na Tanzania. Ni mradi wa kuchimba na kusafirisha mafuta kwa njia ya bomba linalolazwa ardhini, kuanzia visima vitakavyokuwa Ziwa Albert, eneo la Hoima, hadi eneo la Chongoleani, iliko Bandari ya Tanga, nchini Tanzania.

Wabia muhimu katika mradi huu ni kampuni ya Mafuta ya TotalEnergies kutoka Ufaransa, Kampuni ya Taifa la China ya Kuchimba Mafuta (CNOOC), Kampuni ya Uganda ya Kuchimba Mafuta, na Shirika la Maendeleo ya Mafuta Tanzania (TPDC). Mradi wa Eacop unatarajiwa kukamilika mwaka 2025.

Bomba la Eacop lina urefu wa kilomita 1,443 kuanzia Kabaale, wilaya ya Hoima, nchini Uganda hadi kwenye Bandari ya Tanga, kwenye Peninsula ya Chongoleani. Karibu asilimia 80 ya bomba hili itatandazwa katika ardhi ya Tanzania.

Mafuta yanayotarajiwa kusafirishwa yatachimbwa kutoka ufukwe wa Ziwa Albert, wenye urefu wa kilomita 160, kwenye mwambao nchini Uganda.

Matokeo ya utafiti uliofanywa na kampuni za kimataifa za utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi za Total, Tullow na CNOOC ulibaini uwepo wa mafuta ghaflitri bilioni 6.5.

Ujenzi wa mradi huo utagharimu Dola za Marekani Bilioni 3.55 na kwamba unatarajiwa kusafirisha mapipa laki 2 ya mafuta kwa siku. Na wakati wa ujenzi wake unatarajiwa kuzalisha ajira kati ya 6,000 na 10,000.

### Montini: Sheria ya ndoa na uzazi - 2

Na Deusedith KAHANGWA

**K**wa sababu ya mabadiliko kyanayotokea mwilini kupitia mduara wa mwitikio wa kingono, ngono ya jenitalia kwa jenitalia wakati mwingine ni sababu ya utulivu wa kimwili na kiakili.

Kwa hivyo, wakati mwingi, ngono ya jenitalia kwa jenitalia ni alama ya utulivu wa kimwili na kiakili, kwa maana kwamba utulivu wa kimwili na kiakili.”

Na kwa sababu hii ni suluhisho dhidi ya ukengefu wa kijamii wenye sura ya uasherati, uzinzi na upigaji wa punyeto, tabia ambazo zinavunja utulivu wa kimwili na kiakili.

Hadi hapa, tunaweza kusema kwamba, ngono ya jenitalia kwa jenitalia inayo malengo matatu.

Kuna kazi ya uzazi, kazi ya kuwakutanisha watu wawili, kwa kuweka muungano wa kudumu kati yao; na inaleta hisia za burudani ambazo zinaweza kuleta utulivu wa kimwili na kiakili.

Nne, ni “hoja kuhusu upekee wa kingono,” ambayo inasema kwamba, kwa kuzingatia kanuni ya kujitoa kama zawadi kamili katika ndoa, wanandoa hujenga mahusiano ambayo ni kati ya watu wawili pekee. Mahusiano kama vile uasherati na uzinzi ni mahusiano yanayojumuisha watu wengi, na hivyo tofauti na ndoa.

Tano, ni “hoja kuhusu uwezekano wa maisha ya pamoja kudumu hadi kifo kinapowatenganisha wahusika,” ambayo inasema kwamba, kinyume na ndoa inayoeleweka kama ahadi ya maisha yote kwa manufaa ya watoto na wanandoa, matendo ya ngono kama vile uasherati na uzinzi ni mahusiano ya muda mfupi kwa manufaa ya wenza pekee.

Sita, ni “hoja kuhusu ya ahadi kati ya wahusika,” ambayo inasema kwamba, ndoa inatokana na ridhaa huru kati ya mwanamume na mwanamke walioahidiana kuishi kama mke na mume, kila mmoja akiwa amefungwa na haki na majukumu maalum kwa mwenzake.



Montini

Saba, ni “hoja kuhusu mafungamano mapana,” yaani “broad inseparability thesis,” ambayo ni kama ifuatavyo:

Mahusiano ya kijinsia yatakuwa na sifa ya kuitwa ndoa endapo tu yanadhihirisha sifa tano kwa wakati mmoja. Sifa hizo ni alama ya umoja, alama ya uzazi, upekee wa kingono, na uwezekano wa maisha ya pamoja kudumu hadi kifo kinapowatenganisha wahusika.

Kinyume chake, mahusiano ya kimapenzi yatakuwa sio ndoa ikiwa tu hayana angalau moja ya sifa hizi tano. Kwa hiyo, fasili ya Montini ni fasili inayofanikiwa kutueleza ndoa ni kitu gani na sio kitu gani. Yaani, “necessary and sufficient definition of marriage.”

Kwa mtazamo huu, kama tendo la ngono ya jenitalia kwa jenitalia likichukuliwa kama alama asilia yenye maana tatu, yaani maana ya umoja, maana ya uzazi na maana ya utulivu, basi, kiunganishi cha maana hizo ni ndoa yenyewe, kama ilivyochaguliwa kwa hiari na wahusika.

Kwa maana hii, tunaweza kusema pamoja na Montini kwamba, kama ndoa ikichukuliwa kama alama yenye maana ya umoja, maana ya uzazi, maana ya utulivu,

*Itaendeela wiki ijayo...*

## Bella 9: Msaanii asiyependa 'kiki'

Na Shabani LULELA

**P**AMOJA na kuwepo ukweli kwamba wasanii wengi Afrika wanapenda “kiki,” lakini wale walioko Tanzania wanaweza kuvuka viwango vya kijimwambafai – kama vipo.

Kiki ni neno maarufu likitumika kwa wale wanaopenda kujionyesha kwamba wana mafanikio lakini ukweli ni kuwa hawana.

Wasanii wa Tanzania wanaelezwa kupenda kujidai wanamiliki pesa nyingi, magari, majumba na hata wapenzi wengi, lakini ukweli ni kwamba wengi wao ni kapuku. Hawana vitu wanavyodai kwamba ni vyao.

Walio kwenye kundi la kupenda kiki zaidi ni wasanii wa Bongo Flewa. Hawa wako radhi kudanganya dunia kwamba wanamiliki hiki ama kile, ilimradi waonekane ‘wamepambana’ kwa kiasi kikubwa hata kufanikiwa, lakini ukweli ni kwamba hawana kitu.

Kumuona msanii wa kike anajitangaza kununuliwa gari la kifahari ama kununua mwenyewe, siyo habari tena. Kusikia msanii wa kiume ana miliki magari yanayoonekana kumilikiwa na matajiri wa Ulaya na Marekani, siyo ‘ishu’ tena Tanzania.

Hawa wote hawashindani kwa kutunga mashairi ya maana ama kuwa na mtiririko mzuri wa vyombo katika nyimbo zao au muonekano mzuri wa video zao, wao wamekalia kusutana nani ana pesa nyingi ama nani ana mwanamke au mwanamume mzuri.

Kutumia muda mwingi kubishana kwa mali zisizokuwa zao, sasa wamepoteza nguvu ya kuwa na mashairi bora, wamebaki wanaandika na kuokoteza tungo ilimradi watoe albumu. Hakuna tena wanamuziki wenye mantiki. Wote wamebaki kubwabwaja.

Kutokana na majigambo hayo, wapenzi wengi wa muziki, hasa wanaojitambua na wenye kuuthamini muziki kuwa njia ya kuburudisha kistaarabu na kuelimisha,



wamerejea kwenye miziki ya zamani ambako wanapata vionjo vya maana.

Hata hivyo, bado wapo wanamuziki wachache ambao wanajitambua na hawataki kuwa na kiki za kujifanya wao wamepata mafanikio makubwa kupitia muziki wao.

Miongoni mwa wanamuziki hao wachache waliobaki, ni Abednego Damiani, maarufu kwa jina la muziki – Bella 9. Huyu ni msanii mkubwa, kijana kutoka Mtaa wa Mafinga, Morogoro ambaye kwa sasa amehamishia shughuli zake Dar es Salaam.

Akiwa na nyimbo zaidi ya 50; mazikiwa; Sumu ya Penzi na Masogange, Wewe ni Wangu, Nilipe Nisepe, Amerudi, Umenitupa, Ladha ya Mapeenzi, Wewe Nami, House Boy, Wanitaka, Burger Movie Selfie, Umefanana Naye, Vitamin Music, Listen, Shauri Zao, na nyingine nyingi, Bella 9, anasema hajawahi kupenda kiki.

Anasema wanaopenda kiki ni wanamuziki wasiojiamini wala kupenda wanavyomiliki, hivyo anaona kutangaza kumiliki magari ama nyumba za kifahari ambazo siyo mali yako, ni kujilisha upepo.”

Anawaasa wasanii wenzake kufanya kazi kwa bidii, kuwa waaminifu na zaidi sana kumtumainia Mungu katika shughuli zao ili waweze kufanikiwa.

# PICHA KUBWA



*Jua linapoelekea kuzama huleta taswira nzuri ya kuvutia. Hapa ni picha iliyopigwa jana – Septemba 18, 2022 eneo la Ununio, Dar es Salaam wakati jua likikaribia kuzama. (Picha na Simon Mkina).*

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi na Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 00000448.

